

WILAYA YA MARAKWET MAGHARIBI

102/1

KISWAHILI

Karatasi 1

MUDA SAA 1 $\frac{3}{4}$

Julai/Augosti -2015

MAAGIZO

- (1) Andika insha mbili:Insha ya kwanza ni ya **lazima**.
- (2) Chagua insha moja kati ya tatu zilizobakia.
- (3) Kila insha isipungue maneno 400.
- (4) Kila insha ina alama 20.

Maswali.

1. Wewe ni mpenzi na msomaji wa mojawapo wa magazeti nchini. Mwandikie barua mhariri wa gazeti hilo ukitoa maoni yako kuhusu umuhimu wa katiba mpya iliyoidhinishwa hivi majuzi.
2. Fafanua njia mbalimbali za kustawisha michezo nchini.
3. Ivushayo ni mbovu..
4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya;
.....sikuamini niliyoyaona. Nilibaki nikijiuliza, “Ni macho yapi yasiyolengalenga machozi kwa kushuhudia haya?”

WILAYA YA MARAKWET MAGHARIBI

102/2

KISWAHILI

Karatasi 2

MUDA SAA 2 ½

Julai/Augosti -2015

1. **UFAHAMU (Alama 15)**
soma taarifa ifauatayo kisha ujibu maswali

Serikali ya Kenya, imeimarisha mno kampeni dhidi ya vileo na dawa za kulevya nchini. Hii imefanyika kitika viwango vya taasisi na pia mipango.

Historia ya NACADA inaanzia mwaka 1996 wakati kamati ya Uratibu ya Wizara mbalimbali ilipoundwa. Kamati hiyo iliongozwa na wakili mkuu wa serikali ilhali ofisi ya mkuu wa sheria iliendelesha shughuli za kila siku.

Baadaye mwezi Aprili 2001 kupitia tangazo la gazeti rasmi la serikali, shirika la taifa la kupambana na Dawa za kulevya (NACADA) liliundwa. Jukumu lake kuu lilikuwa kuanzisha kampeni ya kuhamasisha umma dhidi ya dawa za kulevya hasa miongoni mwa vijana shuleni. Hii ilitokana na wimbi la mgomo hatari ya wanafunzi na tuhuma za uabudu shetani, ambazo kwa kiasi zilisemekana kuchangiwa na matumizi ya dawa za kulevya.

Kuimarisha hatua dhidi ya dawa zilizopigwa marufuku nchini, serikali ilibadilisha shirika hili likawa mamlaka ya kitaifa ya kupambana na Dawa za kulevya (NACADA) chini ya sheria ya mashirika ya serikali mnamo Juni 2007, na kuyaweka katika ofisi ya Rais, Wizara ya serikali ya Utawala wa mkoa na usalama wa ndani. Jukumu hilo liliwezesha NACADA kusimamia kampeni ya sekta mbalimbali ya kuzuia, kudhibiti na kukabiliana na athari za vileo na dawa za kulevya nchini.

Majukumu ya mamlaka hii yalizidishwa kwa kujumuisha, miongoni mwa wengine, kuwezesha kuundwa, kupewa leseni na kuanzishwa kwa vituo vya kutibu na kurekebisha tabia za waathiriwa: kusimamia mifumo ya kisheria na sera inayolenga kisitisha usambazaji dawa za kulevya na kupunguza hitaji la dawa hizo: kusaidia serikali za kaunti kutekeleza sera na sheria za kudhibiti dawa za kulevya; na kuwasilisha bungeni ripoti mbili kila mwaka kuhusu udhabiti wa vileo na dawa za kulevya.

Wito wa NACADA, Taifa Huru bila Dawa za kulevya, una maono ya taifa lenye wananchi walio na afya bila ulevi na uraibu, kwa hivyo wanaweza kushiriki katika fani zote za ujenzi wa taifa. Ni dhahiri kwamba mtu mlevi ama aliyenaswa na dawa za kulevya hawezi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kuleta maendeleo kama elimu, ukulima, ufugaji, uhufadhi mazingira, utoaji huduma za afya, biashara na kutoa usalama kwa jamii. NACADA inajizatiti kuzuia hali hii na wakati huo ikiweka mikakati ya kukabiliana nayo.

Katika mwongo uliopita, NACADA imehakikisha kwamba; kuzuia na kukabiliana na ulevi na dawa za kulevya kunajumuishwa katika huduma za sekta ya umma ambapo taasisi zote za umma zinaweka mikakati ya kupambana na dawa za kulevya na kisha kutoa ripoti kila baada ya miezi mitatu kwa NACADA.

Pili vijana shuleni na waalimu wao wanahamasishwa kwa lengo la kuwazuia kutumia dawa za kulevya na kuimarisha maisha yao.

Ujumbe mahsusi anaolenga kubadilisha tabia na mitazamo dhidi ya pombe nadawa za kulevya unatayarishwa na kuenezwa kupitia magazeti na vyombo vya habari vye elektroniki kama televisheni na radio.

Aidha kampeni ya hamasisho dhidi ya dawa za kulevya inayolenga makundi yaliyo katika hatari zaidi inafanywa kupitia mbinu mbalimbali zikiwemo warsha,michezo,misafara ya barabarani na mitandao ya mawasiliano.Baadhi ya makundi haya yaliyofikiwa na NACADA ni wanaojidunga sindano za dawa za kulevya,madereva wa malori ya masafa marefu,wahudumu wa matatu na bodaboda,walemavu,vijana katika mitaa duni,na wale wanaopitia tambiko za kitamaduni.

Kampeni hii hata hivyo imejaa changamoto si haba.Kuu zaidi ni viwango vya juu vya bidhaa hizi hasa miongoni mwa vijana.Urahisi ambao pombe na dawa zingine zinapatikana hata na walio katika hatari kudhuriwa kumechangia matumizi ya bidhaa hizi hivyo kurejesha nyuma kampeni hiyo.Hii ni pamoja na mbinu hafifu za kukomesha uraibu huu ikiwemo upungufu katika utekelezaji wa sheria na upungufu wa uwezo wa kufuatilia kunatoka mihadarati na kule zinakosafirishwa na walangizi.

Changamoto nyingine ni vileo visivyodhibitishwa kisheria kama vile miraa na muguka,ambavyo vin athari kubwa kwa wanaozitafuna.pia dawa ya ki – afya kama vile diazepam na valium ambayo yanatumiwa vibaya na waraibu hususan vileo.

Kizuzi kingine kikubwa ni kimya na kukana kuwepo kwa tatizo hili hasa na waathiriwa,jamii na wanafunzi.Hii inawazuia wanaoadhiriwa,na uraibu huu kutafuta tiba,kurekebisha tabia na usaidizi wa kijamii.Taifa pia halina huduma za kutosha za matibabu na kurekebisha tabia.Vituo vingine ni vya kibinafsi na hutoza gharama na juu sana na hivyo kufanya mwananchi wa kawaida kutovifikiria.

Kampeni kuingiliwa na wadau na changamoto nyingine.Kwa mfano sekta ya pombe imeendelea kuwasilisha kesi mahakamani kupinga utekelezaji wa sgeria ya kudhibiti vileo,2010.pia imeweka matangazo ya kuchochea yasiyona maadili kwa lengo la kuongeza unywaji wa bidhaa zao hata na makundi yaliyo katika hatari ya kuadhuriwa bila kuzingatia kanuni bora zinazotumika kote duniani.

NACADA hivi sasa imo katika harakati za kupata uungwaji mkono ili kutangaza pombe na dawa za kulevya kama janga la kitaifa ili kuchochea kuwekwa kwa mikakati inayotosha kukabiliana na tatizi hili.

Mipango inafanywa kuhusisha utaalumu katika vita hivi kwa kuunda mitaala ya masomo katika viwango vya cheti,diploma,digrii na shahada ya pili.Hili linafanywa kwa ishirikiano na vyuo vikuu vya umma hapa nchini.

Maswali

- (a) Ni nini msingi wa NACADA? (alama 2)
- (b) Fafanua azma ya kuasisiwa kwa NACADA . (alama 2)
- (c) Mabadiliko ya mwaka 2007 yalizidisha wajibu wa mamlaka.Fafanua. (alama 3)
- (d) Eleza athari hasi kwa aliyemraibu wa vileo. (alama 2)
- (e) NACADA imefaulu kiwango Fulani katika kampeni zake.Thibitisha. (alama 2)
- (f) “Barabara ndefu haikosi kona”.Thibitisha ukweli wa methali hii kwa kurejelea juhudi za mamlaka ya NACADA. (alama 3)
- (g) Eleza maana ya neno mwongo kama lilivyotumika taarifani. (alama1)

2. MUHTASARI

Kila mwaka, watoto milioni 10 hufariki katika mataifa yanayoendelea kabla ya kifikisha umri wa miaka mitano. Hii mara nyingi hutokana na wagonjwayanayoweza kuzuiliwa ama kutibiwa. Kulingana na ripoti ya hivi punde kabisa ya shirika la watoto la umoja wa kimataifa UNICEF, watoto milioni 2.2 wanaweza kuokolewa ikiwa wazazi wao watahudhuria kliniki inavyohitajika baada ya kujifungua hadi miaka mitano. Huu ndio wakati watoto hupewa huduma muhimu kama chanjo. Vilevile, mzazi hupokea mawaidha muhimu kuhusu jinsi anavyoweza kumlea mwanawe katika hali nzuri, na hatua anazohitajika kuchukua shida zinapotokea.

Kliniki hizi ni muhimu sana haswa kwa kutoa mwongozo jinsi yakumtunza mtoto na mama mwenyewe baada ya kujifungua. Huduma anazopata katika kliniki hukuwezesha kutambua ikiwa mwanao anakua ipasavyo na hatua utakazochukua tatizo linapotokea. Sababu kuu ni kwamba miaka mitano ya kwanza katika maisha ya mtoto ni kipindi kinachohitaji mzazi kuwa muangalifu sana. Kipindi hichi ambacho wataalamu hukiita pre-school health ni muhimu mno kwani mtoto hukaguliwa namna anavyokua na hali yake ya afya. Hakuna mwingine anayefahamu afya ya mwanao vizuri muda wote huu ila muuguzi anayekuhudumia katika kliniki baada ya kujifungua.

Hata hivyo wataalamu wanasisitiza kwamba kliniki si kwa kina mama pekee bali kwa wazazi wa kiume. Kina baba wanahimizwa wahudhuria kliniki hizi kwani jukumu la kumlea mtoto ni la wazazi wote wawili.

Katika kliniki hizi mzazi hupewa habari kuhusu maradhi yanayojitokeza katika miezi ya kwanza kama homa ya macho, vipete vya ngozi, uvimbe wa ndani, kuhara, kulia ovyo ovyo na msokoto wa tumbo. Lakini si hayo tu utapata ufahamu wa magonjwa sugu ambayo UNICEF inaorodhesha kama sababu kuu zinazopelekea watoto wengi kaatika nchi zinazoendelea kufariki wakiwa chini ya miaka mitano. Virusi vya HIV na Ukimwi, surua, malaria, kuharisha na nimonia husababisha asilimia 3, 4, 8, 17 na 19 mtawalia ya vifo hivi. Hata hivyo maradhi yanayotokana na hali mbaya ya mama anapomtunza mwanawe, au mazingira machafu husababisha vifi asilimia 36 ama milioni 4 katika mwezi wa kwanza baada ya kuzaliwa. Nao ugonjwa wa utapia mlo huwaua watoto milioni sita au asilimia 53 kila mwaka. Mzazi anapaswa kujihami na ufahamu wa maradhi haya ambayo mengi hupuuza kama maambukuzi rahisi. Wale wanaopuuza kliniki hizi baada ya kujifungua huwa wanajihatarisha kando na kujionyesha kama wazazi wapumbavu ilhali wanaelewa majukumu yao.

Nchini Kenya, changamoto kuu katika miaka kuhakikisha watoto wanakua na kufikisha miaka mitano wakiwa wenye afya bora ni kutolewa kwa huduma za kimsingi kwa watoto wote kokote kule. Serikali inajitahidi kuimarisha kampeni za kuwasihia kina mama kuhudhuria kliniki baada ya kujifungua. Utawapata wahudumu wa afya tayari kukupa mawaidha jinsi ya kuzuia magonjwa kadha ambayo huwatatiza kina mama na hata kutoa matibabu ya kwanza kwa yale maradhi mwanao atapata.

Kumekua na matangazo ya mara kwa mara katika vyombo kuhusu chanjo za bure zikitolewa mle mashinani na maafisa wa afya wa serikali. Katika mataifa kadhaa serikali zimeongoza uwezekano wa kufikia na kupokea huduma za afya kwa kuondoa ama kupunguza gharama za huduma msingi katika vituo vya umma. Aidha serikali zimeimarisha ubora wa huduma zinazotolewa kwa kuwapa mafunzo maafisa wa afya. Pia, zinawapa mafunzo watu kutoka jamii hizi waliojitolea kufikia jamii zilizo mbali na kliniki. Hivyo wanaweza kutoa ushauri kuhusu jinsi ya huduma ya kwanza kutibu magonjwa haya watu huwa wa kujitolea huwa muhimu sana katika kuripoti visa vya mkurupuko wa maradhi kwa maafisa wa afya kwenye kliniki za kina mama na watoto. Njia ya pili inayotumika kwa wingi ni kampeni za chanjo zinazoendeshwa na serikali kwa usaidizi wa wakaazi wa maeneo hayo ili kuhakikisha kila mtoto

- (a) Kwa maneno 40 – 45 dondoa hoja kuu katika aya tatu za kwanza.(alama 6, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

Nakala safi

- (b) Fupisha aya tatu za mwisho.(maneno 80)
(alama 9,1 ya mtiririko)

Nakala safi

3. **MATUMIZI YA LIGHA:(Alama 40)**

- (a) Tunga sentensi ukitumia vinyume vya maneno yafuatayo (alama 2)

afikiana

hitimisha

- (b) Kwa mtindo wa visanduku ichanganue sentensi hii. (alama 4)

Amejenga nyumba nzuri lakini Kombo amejenga nyumba ndefu.

- (c) Fafanua matumizi matatu ya kistari kirefu. (alama 3)

- (d) Ainisha mofimu katika neno hili. (alama 3)

Watupikiao

- (e) Onyesha kirai – husishi katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Wanafunzi walienda mjini kwa miguu kurejea jioni hiyo.

- (f) Andika sauti zifuatazo. (alama 2)

(i) kikwamizo Hafifu cha kaakaa gumu.

(ii) kipasuo ghuna cha midomo – meno.

- (g) Usipokesha hutasinzia darasani na utasoma vizuri.(yakinisha katika wingi)
(alama 2)

- (h) Bainisha dhana zinazojitokeza katika sentensi zifuatazo ukizingatia vitenzi. (alama

2)

- (i) Wazee walinywea kata
- (ii) Mhalifu ananywea gongo chini ya mnazi

- (i) Andika nomino zinazotokana na maelezo yafuatayo. (alama 2)
 - (i) Kuondoa baadhi ya fonomu kutoka kwa kitenzi
 - (ii) Kutobadilisha fonimu yoyote.
- (j) Tunga sentensi kuonyesha chagizo. (alama 2)
- (k) Andika sentensi mbili ukutumia viunganishi viteuzi. (alama 2)
- (l) Fafanua matumizi mawili ya hali ya a. (alama 2)
- (m) Geuza sentensi hizi ziwe katika kauli zilizo kwenye mabano. (alama 2)
 - (i) Ufisadi umeifilisi kampuni yao iliyokuwa kubwa.(kitendwa)
 - (ii) Wenzake wamemdharau tangu siku hiyo.(kutendeka)
- (n) Eleza matumizi ya na katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
 - (i) Fahamu daima kwamba mla nawe hafi nawe.
 - (ii) Alikaripiwa na mamake alipokosa
- (o) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi wa taarifa. (alama 2)

“Nimeitwa katika kituo cha polisi,sijui nitarejea lini.Nakuomba uniangalilie nyumba hadi nitakaporudi”,Bi Ketu alimwomba mama Tatu.
- (p) Huku ukitoa mifano fafanua vipashio vya lugha. (alama 2)
- (q) Andika maneno yenye utaratibu ufuatao. (alama 2)
 - (i) KIKKKI
 - (ii) KKKIKI
- (r) Geuza iwe katika ukubwa. (alama 2)

Mtwana huyu aliwabeba wana wa kidudu kisha wakafungua duka.
- (s) Tumia neno kama kuikanusha sentensi ifuatayo. (alama 1)

Ukiwabughudhi wanawake unajidunisha.

4. **ISIMU JAMII** (alama 10)

Jadili sababu tano zilizochochea usanifishaji wa Kiswahili.

WILAYA YA MARAKWET MAGHARIBI

102/3

KISWAHILI

FASIHI

Karatasi 3

MUDA SAA 2 ½

Julai/Augosti -2015

MAAGIZO

- (a) Jibu maswali manne.Sura la Kwanza ni LAZIMA.
- (b) Usijibu maswali mawili kutoka kitabu kimoja.
- (c) Mtahiniwa aangalie na kuhakikisha kuwa maswali yote yapo

SWALI LA LAZIMA

SEHEMU YA A (RIWAYA) UTENGANO: SAIDA M.)

SEHEMU YA A. (RIWAYA) UTENGANO: SAIDA M.)

- a) Malaika nakupenda malaika,
Nami nifanyeje, kijana mwenzio
Nashindwa na mali sina we,
Ningekuoa malaika
 - i) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)
- b) Wimbo unaofuata baada ya wimbo wa dondoo hilo unatajwa kama wimbo wa sadfa ya yaliyomo. Eleza (al.2)
- c) Eleza miktadha mingine miwili tofauti ambayo nyimbo zimetumika. (al.2)
- d) Kwa kila wimbo uliotaja hapojuu eleza malengo ya kila wimbo huo (al.4)
- e) Ndoto za Maimuna ni jazanda na ubashiri wa maisha yake. Eleza. (al.8)

SEHEMU YA B: DAMU NYEUSI- Ken Walibora na Ahmed Said

2. Umaskini ndicho kikwazo kikuu cha maendeleo. Ukirejelea hadithi zozote tano katika diwani ya

Damu Nyeusi na hadithi nyingine, thibitisha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

Au

3. ‘Ukumbi ulivuma kwa mtu na muziki,seuze machupa ya soda,bia,mvinyo na vinywaji vingine kemkem? Vyote hivyo vikaonekana kushiriki kikamilifu katika dhifa ile.’ **MIZIZI NA MATAWI**

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili- (alama4)
- b) Taja mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama2)
- c) Eleza sifa za anayerejelewa (alama 6)
- d) Fafanua maudhui yoyote matatu katika hadithi husika (alama6)
- e) Eleza hatima ya wahusika katika hadithi hii (alama 4)

SEHEMU YA C: MSTAHIKI MEYA-Timothy Arege

4. Hawa wanaotaka uwasikilize ni mzizi wa vizazi vya kesho! Yote yanategemea uwezo wetu...

- i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- ii. Eleza hulka nne za msemaji (alama 8)
- iii. Eleza yanayotokea baada ya dondoo hili. (alama 6)
- iv Eleza mbinu kuu ya lugha iliyotumiwa kwa dondoo hili. (alama 2)

Au

5. Mwananchi huivunda nchi yake mwenyewe. Jadili ukweli wa kauli hii ukirejelea tamthilia (alama20)

SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI

RASHID NA ZIMWI MTI

Hapo kale palikuwa na mfalme mmoja aliyekuwa na binti mrembo sana. Watu chungu nzima vijana na hata wazee walitamani kumuoa lakini hawakufanikiwa. Sio kwa vile tu alikuwa mrembo lakini alisemekana kwamba atakayemwoa binti yule wa uzuri, basi siku moja atarithi baba yake na kuwa mfalme wa nchi nzima. Mfalme mwenyewe alikuwa nadhiri kwamba mtu yeyote yule ambaye angaliweza kujibu swali lake, basi angalimuoia bintiye. Swali lenywe ni hili:-

“Kati ya vitu vyote katika ulimwengu, je ni kitu gani ambacho ni kasi kuliko vyote. Kitu chenyewe tunakidhamini zaidi wakatitulia nacho kuliko wakati ambao hatunacho. Kituambacho huleta uhai kwa walio Wachanga na kifo kwa walio wazee?”

Watu wengi walifika kwa mfalme kila siku kujaribu bahati yao lakini wapi. Hakuna aliyeweza kufua dafu.

Basi katika nchi ile, palikuwa na Kijana mmoja aliyeitwa Rashid. Yeye alikuwa na shamba lake dogo nje ya nyumba yake na alikuwa bado hajapata jiko. Rashidi hakutaka kujisumbua kutafuta jibu Ia swali Ia mfalme kwani alijiona mwenye dosari hivyo hangaliweza kumwoa binti mfalme,kwa vyovyote vile. Basi kila siku alikuwa akifanya kazi shambani mwake.

Katikati ya, shamba lake palikuwa na mti ambao ulionekana kukua kila siku. Basi siku moja aliazimia kuukata mti ule. Alienda akachukua shoka lake na kulinoa vikali kisha akaja kuukata.

“Mwanadamu, tafadhali usinikate”, mti ulisema

Rashidi aligutuka sana na akasimama kando akiduwaa.

“wewe ni nani?” Rashidi akauliza.

“Mimi ni zimwi mti”, mti ukajibu

Sina budi kukukata kwani uko shambani mwangu nawe wanizuia nikifanya kazi yangu”,

Rashidi alijibu.

Aliinua shoka lake tena tayari kuukata lakini mti ukasema kwa sauti ya unyenyekevu

“Tafadhali nihurumie nami nitakufanyia kazi yoyote utakayoniambia”.

Rashidi alifikiria kidogo na kusema, “Mimi nina swali hapa na siwezi kulitua, je waweza kuniambia jibu lake?”

‘Haya mwanadamu, hebu uliza, kama siwezi basi tutaenda kwa ndugu zangu katika nchi ya kuzimu, au kwa mizimu ya anga au kwa mizimu ya wafu na bila shaka tutapatajibu la swali lako. Haya sasa niko tayari kulisikiliza”.

Rashidi alimwambia lile swali la mfalme lakini lile zimwi mti halikuweza kujibu. Basi hapo walifunga safari kuelekea katikati ya dunia. Walipita miomba na mail na hatimaye walifika.

“Usiwe na hofu kwani mimi nitakulinda”. Zimwi lilisema.

Walikaa mle kwa muda wa miaka mingi lakini hawakupata jibu lile. Kisha walienda kwa mizirnu ya anga lakini wapi. Hatimaye walienda kwa wafu. Huko Rashidi aliona kila ama ya watu. Wale waliokufa wakiwa wema, wabaya, waliouwawa vitani na pia wale waliokufa kwa amani vita ndani mwao.

Baada ya kukaa huko kwa muda usiojulikana, Rashidi alilipata jibu kwa kusikiliza mazungumzo juu ya mafumbo na methali baina ya ile mizimu. Basi alifurahi sana kisha akaliambia lile zimwi mti warudi tena duniani kwani alishapata alichotaka. Waliaga na kuanza safari yao ya kurudi duniani. Baada ya safari ndefu walifika tena duniani.

Rashidi alimwacha yule rafikiye zimwi mti pale pale shambani na kwenda kwa mfalme. Watu wengi walishangaa sana kumuona na wengi wao walidhani kwamba alikuwa kizuka.

Basi alimwelezea mfalme yote yaliyotokea. Mfalme alitoa amri mbiu ya mgambo ipigwe na watu wote pamoja na mashujaa wote wakakusanyika kusikiliza hadithi hiyo ndefu na pia kutaka kujua jibu la swali la mfalme kuwajibu la swali lake lilikuwa “WAKATI”.

Mfalme alifurahishwa sana na ushujaaa wa Kijana yule.

Alimwita binti yake ili pia apate kusikia habari hizo.

Baada ya mwezi mmoja arusi ilifanywa na Rashidi akamwoa binti mfalme. Mfalme aliwajengea mahali pazuri pa kukaa na baada ya kitambo kidogo mfalme alifariki na Rashidi akawa mfalme na binti mfalme akawa malkia.

Hadithi hii pia yathibitisha usemi usemao kuwa, bahati ya mtu haichukuliwi na mwingine.” hivyo bahati ya mwenzio, usilalie mlango wazi”. milango ya heri ilikuwa imefungukia Rashidi. Alilala fukara na kuamka mkwasi wa kutajika.

1. a) Taja shughuli moja ya utamaduni na moja ya uchumi wajumuia ya hadithi hii. (alama 2)
- b) Eleza umuhimu wa zimwi mti katika hadithi hii. (alama 4)
- c) Mti unazungumza na binadamu. Hii ni mbinu gani ya sanaa? (alama 1)
- d) Fasiri maana ya “safari” mbili za kwenda kuzimu na kurudi. (alama 4)

- e) Taja visa vinne vya safari zinazoonyesha ushujaa wa Rashidi (alama 4)
f) Taja sifa za utanzu hun wa hadithi. (alama 5)

7. **SEHEMU YA E :(USHAIRI)**

MAHASIMU WA – CHUNGU

Nafungua ruhu yangu, ilofungwa kama fungu
Nieleze kunga zangu, kwawo penda yangu wengu
Waso uso wa maningu, walo nazo hila chungu
Sitishiwi nyungunyungu, wajapojazia chungu

Na wanotumia rungu, kunitisha kwa machungu
Wakamila kilo changu, ela kunipa mizungu
Ntainuka kwa mawingu, na kushinda zao pingu
Sitishiwi nyungunyungu, wajapojazia chungu

Wanofundika makungu, kwa ufundi nende zangu
Wakafunda ndia zangu, maguu angu yanungu
Yatawarudi ya nungu, hawatafikila mbingu
Sitishiwi nyungunyungu, wajapojazia chungu

Pingu chungu kwake mungu, tawa tamu chungu pingu
Damu tamu kwawo yangu, tawa damu tamu chungu
Dawa fungwa ya makungu, tawa iso fungwa kungu
Sitishiwi nyungunyungu, wajapojazia chungu

Wangadaku manzi wangu, asije kuwa mwezi wangu
Wangeleta manza kwangu, kuharibu mwezi wangu
Wangaruka ni vipungu, hawatofika kwa mbingu
Sitishiwi nyungunyungu, wajapojazia chungu

Nyungunyungu waso nyungu, wanajaza changu chungu
Wanafosi jasho langu, na kukila chungu changu
Sitowacha ulimwengu, roho yangu i kwa mungu
Sitishiwi nyungunyungu, wajapojazia chungu

Fungula malango mungu, wasihule moyo wangu
Uyishiye kwa mawingu, unguzila zao rungu
Nipawe mbawa za pungu, wasipate gulu langu
Sitishiwi nyungunyungu, wajapojazia chungu

Namaliza kunga zangu, pa nyasaye pawe pangu
Imetika yao myungu, sitishiwfna miungu
Wajakwenda kwa mangugu, nitafunga tatu nyungu
Sitishiwi nyungunyungu, wajapojazia chungu

© TAIFA LEO 2012

MASWALI

- (a) Shairi hili laweza kuwekwa kwa habari tatu tofauti. Taja na ueleze. (alama 3)

- (b) Eleza arudhi za utunzi wa beti ya pili. (alama 4)
- (c) Eleza maana ya
- (i) Nipewe mbawaa za pungu, wasipate gulu langu.
 - (ii) Kwawo penda yangu wengu. (alama 2)
- (d) Eleza aina nne za mshairi. (alama 4)
- (e) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya kawaida. (alama 4)
- (f) Mshairi alidhamiria nini kwa kulitunga shairi hili. (alama 3)